

## **MRADI WA USIMAMIZI ENDELEU WA MISITU YA MIOMBO MAGHARIBI MWA TANZANIA KATIKA WILAYA YA MLELE.**

Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Misitu ya Miombo Magharibi mwa Tanzania ni mradi wa miaka mitano ulizinduliwa mwaka 2013. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya nne za Urambo, Uyui na Kaliua za Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Mlele ya Mkoa wa Katavi. Katika wilaya ya Mlele mradi unatekelezwa katika kata tatu za Kamsisi, Inyonga na nsenkwa zenye vijiji tisa vya Inyonga, Kaulolo, Nsenkwa, Kamsisi, Mtakuja, Kalovya, Kamalampaka, Songambele na Imalauduki.

Mradi huu unafadhiliwa kwa pamoja na Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF), Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Lengo kuu la Mradi huu ni kuwa na Usimamizi Endelevu wa Misitu ili kulinda mfumo wa Ikolojia na Bayoanuai na kuwa kinga kwa Misitu ya mvua ya Kongo, kuwa na usalama wa chakula na maisha bora kwa wananchi.

Lengo mahususi la Mradi ni kuwezesha jamii zinazoishi kandokando ya misitu kwa kutegemea misitu kuwa na njia mbadala za uzalishaji ambazo ni rafiki kwa mazingira na zitakazo boresha hali ya maisha ya jamii hizo.

Misitu ya Miombo inachukua sehemu kubwa ya eneo la wilaya ya mlele ina manufaa mbalimbali kwa jamii zinazoishi kandokando ya misitu hiyo na kwa taifa kwa ujumla, kwa kuwa ni chanzo cha Nishati kama Kuni na Mkaa, chanzo cha bidhaa muhimu kama Mijengeo, Nguzo, Mbao, Vyombo vya nyumbani, Chakula, Madawa na Malisho. Pia misitu hii hutoa huduma za kiiokolojia kama Makazi ya viumbe hai na kutunza hewa ukaa hivyo kurekebisha athari za mabadiliko ya tabia nchi, kuzuia mmomonyoko wa udongo, chanzo cha kivuli, kuboresha mzunguko wa haidrolojia na kutunza rutuba ya udongo.

Pamoja na kuwa na manufaa yote hayo, Misitu ya miombo imekuwa ikiharibiwa kwa kasi na shughuli mbalimbali za binadamu kama ukataji miti hovyoy, uvamizi wenye lengo la kuanzisha makazi ndani ya misitu, kilimo cha kuhama hama na uanzishwaji wa mashamba katika maeneo ya misitu, uvunaji wa mbao na magogo, uvunaji wa kuni kwa ajili ya kukaushia tumbaku, uchomaji mkaa, mabadiliko ya tabia nchi n.k.

Suluhu ya muda mrefu kwa uharibifu wa misitu hii ni kutwaa desturi ya usimamizi na matumizi endelevu na kudhibiti shughuli za kibiashara za rasilimali hizi kitu ambacho mradi huu unatekeleza.

Mradi huu unatekelezwa kupitia vipengele vikuu vinne ambavyo ni;

- 1 Urekebishaji wa sera na mpangilio wa taasisi kusaidia usimamizi endelevu wa misitu.
- 2 Kuimarisha ujuzi na uwezo wa maarifa kwa usimamizi wa misitu ya jamii/ usimamizi shirikishi wa misitu, usimamizi wa rutuba ya udongo na matumizi bora ya ardhi.
- 3 Uzalishaji endelevu wa mkaa na nishati mbadala ili kupunguza msukumo katika uvunaji wa misitu.
- 4 Kusaidia masoko na teknolojia kwa ajili ya kupunguza msukumo wa uharibifu katika kilimo na rasilimali asili na kuongeza kipato.